PRESS RELEASE

PR23/50

# Taarifa kwa Vyombo vya Habari

# Bodi Tendaji ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Imekamilisha Mapitio ya Kwanza ya Mpango wa Utoaji Mikopo wa ECF (Extended Credit Facility) Pamoja na Majadiliano kwa Mwaka 2023 Chini ya Kanuni ya Nne ya Mkataba Ulioanzisha Shirika hilo (Article IV Consultation)

**FOR IMMEDIATE RELEASE**

- *Leo, Bodi Tendaji ya IMF imekamilisha mapitio ya kwanza ya Mpango wake wa ukopeshaji wa ECF na majadiliano kwa mwaka 2023 chini ya kanuni ya nne ya mkataba ulioanzisha shirika hilo. Kupitishwa kwa mapitio ya kwanza kumeruhusu kutolewa mara moja kwa msaada wa kifedha wa kiasi cha SDR milioni 113.37 (kama dola za marekani milioni 153).*
- *Mpango wa mageuzi ya uchumi wa Tanzania unaendelea vizuri katika mazingira yenye changamoto zitokanazo na uchumi wa dunia na serikali imeendelea na nia yake ya kutekeleza mpango wa ECF*
- *Mageuzi yanalenga katika kuimarisha ufufuaji wa uchumi, kuhifadhi uthabiti wa uchumi mkuu, na kusaidia mageuzi ya kimuundo ili kuleta ukuaji wa uchumi endelevu na shirikishi.*

**Washington, DC - Aprili 24, 2023:** Leo, Bodi Tendaji ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) imekamilisha mapitio ya kwanza ya Mpango wa Utoaji Mikopo wa ECF (Extended Credit Facility) na majadiliano kwa mwaka 2023 chini ya kanuni ya nne ya mkataba ulioanzisha shirika hilo (Article IV Consultation). Kukamilika kwa mapitio ya kwanza kunaruhusu kutolewa mara moja kwa SDR 113.37 milioni (kama dola za Marekani milioni 153), na kufanya jumla ya fedha ambayo hadi sasa imetolewa kwa Tanzania chini ya mpango huu kufikia dola za Marekani milioni 304.7.

Mpango huu wa miaka mitatu wa ECF ulioidhinishwa tarehe 18 Julai mwaka 2022, utaiwezesha Tanzania kupata jumla ya SDR 795.58 milioni (sawa na asilimia 200 ya uwekezaji wa Tanzania IMF  na dola za Marekani milioni 1,046.4 wakati huo mpango ulipoidhinishwa). Mpango huo unalenga kusaidia ufufuaji wa uchumi, kuhifadhi uthabiti wa uchumi mkuu, na kuleta ukuaji wa uchumi endelevu na shirikishi. Mageuzi yanahusu kuongeza nafasi kwenye matumizi ya serikali ili kuruhusu matumizi katika sekata za kijamii yanayohitajika sana na uwekezaji wa umma wenye tija, kuimarisha mfumo wa sera ya fedha na kuboresha usimamizi wa sekta ya fedha, na kuendeleza mageuzi ya kimuundo.

Mpango wa mageuzi ya uchumi wa Tanzania unaendelea. Vigezo na masharti yaliyowekwa kwa  Desemba 2022 yalifikiwa. Masharti ya mageuzi ya kimuundo ya kuandaa na kuanza kutekeleza mpango wa kulipa malimbikizo ya madeni yote na kuwasilisha marekebisho ya sheria ya Benki na Taasisi za Fedha Bungeni yalikamilishwa kabla ya muda uliopangwa. Masharti ya kukamilisha na kuchapisha ripoti ya ukaguzi wa matumizi ya fedha zilizotolewa na

IMF kwa ajili ya kukabiliana na janga la UVIKO-19 na kuwasilisha bajeti ya awali ya mwaka wa fedha 2023/24 Bungeni yalikamilishwa kwa kuchelewa.

Bodi Tendaji pia imepitisha majadiliano kwa mwaka 2023 chini ya kanuni ya nne ya mkataba ulioanzisha shirika hilo (Article IV Consultation) na Tanzania.

Athari za vita vya Ukraine pamoja na athari nyingine za ndani ya nchi zimeathiri kuimarika kwa uchumi wa Tanzania kutokana na janga la UVIKO-19. Baada ya kuimarika kwa wastani hadi asilimia 4.9 mwaka 2021, ukuaji halisi wa Pato la Taifa unakadiriwa kupungua hadi asilimia 4.7 mwaka 2022, jambo linaloakisi athari za hali ya uchumi wa dunia na upungufu wa mvua. Kwa 2023, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kukua hadi asilimia 5.2 kadiri bei za bidhaa duniani zitakavyopungua na kuimarika kwa mazingira ya biashara.

Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutoa usaidizi wa muda na kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi ili kukabiliana na athari ya vita vya Ukraine. Ingawa mfumuko wa bei wa Tanzania uko chini kwa kiasi fulani lakini serikali ilichukua hatua kukabiliana na shinikizo la mfumuko wa bei kwa kutoa ruzuku ya muda kwa bei ya mafuta na mbolea na kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi. Rasimu ya bajeti ya serikali ya mwaka wa fedha 2023/24 inalenga kubana matumizi lakini imetoa kipaumbele kwa matumizi katika sekta za kijamii.

Kutokana na majadiliano kwenye Bodi Tendaji, Bi. Antoinette Sayeh, Naibu Mkurugenzi Mtendaji na Kaimu Mwenyekiti, alitoa taarifa ifuatayo:

“Mpango wa mageuzi wa Tanzania unaoungwa mkono na Mpango wa Utoaji Mikopo wa ECF unalenga kukamilisha hatua zilizochukuliwa ili kukabiliana na madhara ya kiafya na kiuchumi yaliyotokana na janga la UVIKO-19, kulinda utulivu wa uchumi jumla, na kushughulikia changamoto za muda mrefu ili kusaidia ukuaji wa uchumi endelevu na shirikishi, kwa kutumia vipaumbele vya mageuzi vya serikali vilivyoainishwa katika Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa.

“Serikali ya Tanzania imeendelea kuzingatia mpango wake wa mageuzi ya kiuchumi licha ya mazingira magumu ya kiuchumi duniani. Utekelezaji wake umekuwa mzuri sana. Malengo yote yaliyowekwa hadi kufikia mwezi wa Desemba 2022 yalifikiwa, na malengo viwili kati ya matatu ya mageuzi ya kimuundo kwa Desemba 2022 yalikamilishwa kwa wakati.

“Juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuboresha ufanisi wa matumizi zitasaidia kuongeza matumizi ya serikali na hivyo kuongeza uwekezaji kwenye miradi ya kipaumbele na matumizi kwenye sekta za kijamii wakati huo kuendelea kulinda uhimilivu wa deni la taifa. Kuimarisha usimamizi wa mashirika ya umma ni muhimu ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza kwenye bajeti ya serikali. Kwa kuzingatia maendeleo ya hivi karibuni katika kuhakiki malimbikizo ya madeni ya ndani, serikali inapashwa kulipa madeni yaliyohakikiwa na kuepuka kulimbikiza madeni mapya kwa kuimarisha usimamizi wa fedha na kudhibiti ahadi za matumizi. Ingawa hatari ya deni la Tanzania bado ni ya wastani, ni muhimu kuendelea kuweka kipaumbele katika kukopa mikopo yenye masharti nafuu na kuhakikisha kwamba athari zinazoweza kujitokeza kutoka kwenye madeni yenye dhamana ya serikali zinadhibitiwa vyema.

“Wakati mfumuko wa bei ukiendelea kuwa chini ya lengo, Benki Kuu ya Tanzania inapaswa kuwa tayari kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi kadiri itakavyohitajika huku ikiruhusu kubadilika zaidi kwa viwango vya ubadilishaji fedha kulingana na athari za kutoka nje ya nchi. Kukamilisha matayarisho yanayoendelea ya kuhamia kwenye utaratibu wa sera ya fedha inayozingatia viwango vya riba ni muhimu ili kuimarisha ufanisi wa sera ya fedha. Kuboresha

mfumo wa usimamizi wa fedha, ikijumuisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye Mpango wa Tathmini ya Sekta ya Fedha (FSAP-Financial Sector Assessment Program) kutasaidia kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha na kukuza sekta hiyo.

“Mageuzi ya kimuundo ni muhimu ili kukuza ukuaji wa uchumi jumuishi, thabiti na endelevu. Mageuzi kwenye mfumo wa ufanyaji biashara yanapaswa kuzingatia kurahisisha taratibu zenye urasimu, kurahisisha udhibiti wa biashara, na kuimarisha uwazi kwenye udhibiti. Utekelezaji wa mkakati wa serikali wa kupambana na rushwa na kuanzisha mbinu ya kuthibiti Utakatishaji wa Pesa / Kukabiliana na Ufadhili wa Ugaidi kwa kuzingatia hatari zilizopo itasaidia kuboresha utawala bora na kushughulikia mapungufu katika mfumo wa uthibiti wa Utakatishaji wa Pesa / Kukabiliana na Ufadhili wa Ugaidi wa Tanzania. Uwezekano mkubwa wa Tanzania katika kuathirika na mabadiliko ya tabianchi unahitaji kuongeza uwezo wa kustahimili hali ya hewa kupitia sera za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.”

**Tathmini ya Bodi Tendaji**

Wakurugenzi Watendaji walikaribisha mwitikio wa sera za serikali kwenye madhara ya vita nchini Ukraine na kupongeza utekelezaji mzuri wa mpango wa ECF. Ingawa ufufuaji wa uchumi unatarajiwa kuendelea na mtazamo wa muda wa kati ni mzuri, lakini unaweza kuathiriwa na changamoto za uchumi wa dunia. Katika muktadha huu, ni muhimu sana serikali kuendelea kutekeleza mageuzi yaliyomo kwenye mpango wa ECF ili kuimarisha ufufuaji wa uchumi, kuhifadhi utulivu wa uchumi jumla, na kusaidia ukuaji endelevu na shirikishi. Kuendeleza ushirikiano na usaidizi wa IMF and wabia wengine katika kukuza uwezo wa watumishi wa umma ni muhimu sana.

Wakurugenzi walipongeza mpango wa serikali wa kubana matumizi kuanzia mwaka wa fedha 2023/24, huku ikiendelea kulinda matumizi ya sekta muhimu. Walibainisha kuwa kuongeza nafasi ya matumizi zaidi na kuweka kipaumbele kwenye mikopo yenye masharti nafuu kutaruhusu uwekezaji unaohitajika sana kwenye miradi yenye kipaumbele na matumizi kwenye sekta za kijamii-ikiwa ni pamoja na afya na elimu ili kuwajengea uwezo watumishi-huku ikiendelea kulinda uhimilivu wa deni la taifa. Kwa mantiki hiyo, Wakurugenzi waliihimiza serikali kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuboresha ufanisi kwenye matumizi, hasa kwenye uwekezaji wa umma; kuimarisha usimamizi na uwazi kwenye fedha za umma, ikijumuisha usimamizi madhubuti wa mapato yajayo ya gesi asilia; na kusimamia vyema mashirika ya umma. Huku wakikaribisha maendeleo ya hivi karibuni katika kushughulikia tatizo la muda mrefu la malimbikizo ya madeni ya ndania ya serikali, Wakurugenzi walisisitiza kuwa kuimarisha usimamizi wa fedha na udhibiti wa ahadi za matumizi itakuwa muhimu ili kuzuia ulimbikizaji wa madeni mapya. Wakurugenzi pia wanatarajia kuona utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti ya ukaguzi wa matumizi ya fedha zilizotolewa na IMF kwa ajili ya kukabiliana na janga la UVIKO-19.

Wakurugenzi walikaribisha sera ya fedha yenye kutegemea takwimu na kuihimiza Benki Kuu ya Tanzania  kuwa tayari kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi endapo athari za mara ya pili za mfumuko wa bei zitatokea. Walipongeza juhudi zinazoendelea katika kuboresha mfumo wa sera ya fedha na kusisitiza umuhimu kwa Benki Kuu ya Tanzania kupunguza kugharamia bajeti ya serikali. Wakurugenzi pia walitoa wito wa kuimarishwa kwa usimamizi wa sekta ya fedha ili iendelee kukua na kuimarika. Kutokana changamoto kwenye uchumi wa dunia, Wakurugenzi walisisitiza umuhimu wa kuruhusu kubadilika zaidi kwa viwango cha ubadilishaji fedha za kigeni, kuimarisha uwazi katika shughuli za mauzo ya fedha za kigeni, na kuhifadhi kiwango kikubwa cha akiba ya fedha za kigeni.

Wakurugenzi walibainisha kuwa mageuzi ya kimuundo ni muhimu ili kukuza uchumi ambao utakuwa jumuishi, thabiti na endelevu. Walisisitiza kwamba kurahisisha taratibu zenye urasimu, kurahisisha utaratibu wa udhibiti wa biashara, na kuimarisha uwazi wa udhibiti kutaleta maendeleo ya sekta binafsi. Pia walisisitiza kwamba kutekeleza mkakati wa serikali wa kupambana na rushwa na kuanzisha mbinu ya kusimamia na kuthibiti Utakatishaji wa Pesa / Kukabiliana na Ufadhili wa Ugaidi kwa kuzingatia hatari zilizopo kutasaidia utawala bora na kushughulikia mapungufu yaliyopo. Kwa kuzingatia uwezekano mkubwa wa Tanzania kukabiliwa na mabadiliko ya tabianchi, Wakurugenzi walitoa wito wa kuongeza ustahimilivu kupitia sera za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinazoungwa mkono na mkakati mpana wa ufadhili. Walizingatia pia dhamira ya serikali ya kupata ufadhili kutoka kwenye mfuko wa RST (Resilience and Sustainability Facility).